# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA NNE

**01 NOVEMBA, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA NNE – TAREHE 01 NOVEMBA, 2024

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa

Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**48. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Ofisi ya Mkuu wa Wilaya pamoja na Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo zitajengwa.

**49. MHESHIMIWA AZIZA SLEYUM ALLY (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Vibali vya Ujenzi hutolewa baada ya muda gani tangu muombaji aombe kupewa kibali.

**50. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatekeleza mkakati wa kujenga Zahanati kwenye Vijiji vyote nchini.

**51. MHESHIMIWA SALIM ALAUDIN HASHAM (ULANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja linalounganisha Kata ya Mwaya na Mbuga lililovunjika tangu mwaka 2023.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**52. MHESHIMIWA OMAR ALI OMAR (WETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mapitio katika kubaini kaya maskini ili kuondoa malalamiko.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**53. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mkakati gani kunusuru vipando visivyohimili maji ya Bahari katika Bonde la Tibirinzi Chakechake Pemba.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**54. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, kwa nini lugha ya Kiswahili haitumiki kwenye Bunge la SADC kama ilivyo kwenye Bunge la PAP ambapo ni lugha rasmi.

**WIZARA YA AFYA:**

**55. MHESHIMIWA NANCY HASSAN NYALUSI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itapeleka mtaji MSD.

**56. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali imejipangaje kuanzisha mpango wa M-Mama katika maeneo ya Kibiti, Mafia na Mkuranga ili kuzuia vifo vya Akina Mama Wajawazito.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**57. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha Wahitimu wa Mafunzo ya Jeshi USU wanapata haki ya ajira sawa na Watanzania wengine.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**58. MHESHIMIWA AGNESTA LAMBERT KAIZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, kwa kiwango gani Sheria zilizopo za kupambana na matukio ya ubakaji zinajitosheleza.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**59. MHESHIMIWA KHAMIS YUSSUF MUSSA (KWAHANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itakarabati Kituo cha Polisi Ng'ambo - Kwahani kwa kuwa ni chakavu na cha muda mrefu.

**60. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kuna mpango gani wa kuunga mkono juhudi za Wananchi wa Kata ya Mdabulo Mufindi wanaojenga Kituo cha Polisi kwa nguvu zao wenyewe.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**61. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itaanza Ujenzi wa Minara ya Simu katika Kata za Nahasey, Gunyoda, Silaloda na Marang - Mbulu Mjini.

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**62. MHESHIMIWA TAUHIDA CASSIAN GALLOS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, kuna mpango gani kuhakikisha Wasanii wanafanya kazi zao kwa uhuru pasipo kuvunja Sheria, Kanuni na Maadili ya Kitanzania.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**63. MHESHIMIWA ABEID IGHONDO RAMADHANI (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, kuna mpango gani kuwakamata na kuwachukulia hatua watu wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

**WIZARA YA KILIMO:**

**64. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imejenga Mabwawa makubwa mangapi nchini.

**WIZARA YA MAJI:**

**65. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha Miradi ya maji inakamilika kwa wakati katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga.

**WIZARA YA UJENZI:**

**66. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX (BUHIGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara inayounganisha Wilaya ya Kigoma Vijijini na Buhigwe itajengwa kwa kiwango cha lami kuanzia Mahembe, Kinazi hadi Buhigwe.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**67. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Bandari mpya ya Mbamba Bay itaanza kujengwa.

## IV. KAMATI YA MIPANGO:

### WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**01 NOVEMBA, 2024** **KATIBU WA BUNGE**